

UJAMA SOCIAL Club katika njia ya Gatundu watakua na Harambee hapo jumapili tarehe 16 Novemba huko Mwembe Tanganyika kuchangisha pesa za ujenzi wa nursery na ukumbi wa Starehe. Picha yaonyesha mchoro wa jumba lenyewe litakapomaliza ambalo litaragiwa kugharimu Shs. 883,000. PICHA: NATIONAL STUDIO

FARSY ATOA MAISHA YA SEYYIDNA HUSSEIN

na SAID BURHAN

KADHI Mkuu wa Kenya Sheikh Abdalla Saleh El-Farsy, ametoa kitabu kipya cha maisha ya Imam Hussein Bin Ali Bin Abitalib, mjukuu wa pili wa Mtume Muhammad (S.A.W.). Kitabu hichi kinatangulia kitabu alichotoa hivi karibuni cha maisha ya Seyyidna Hassan, Khalifa wa mwisho katika wale Makhalifa wa haki watano waliotawala na wakafata sera za mwenyewe Mtume kama alivyowafundisha.

Sheikh Abdalla ni mwanahistoria wa Kiislamu aliyoko katika hali ya juu kabisa, na pia ni mwandishi wa vitabu vya fani mbali mbali vya dini ya Kiislam.

Vitabu vyake vimesambaa Mwambao wote wa Afrika Mashiriki na vyengine viko Arabuni vinasomwa na wanafunzi wa Sheikh Abdalla na hata wale Mustamiin (wasikilizaji) mara nyingi washapata fursa ya kusikia katika darsa za shekhe akitoa Historia ya Kiislamu, kuhusiana na maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W.), wakeze, masahaba zake, jamaa zake na kadhalika.

Pia shekhe Amirijeshi akipiganisha vita hivyo. Ajabu ya Mwanazuoni huyu ni kwamba anaweza kuendesha darsa ya tarehe kwa muda wa masaa mawili bila ya kuangalia kwenye kitabu na ilhali katika maelezo yake atataja majina ya masahaba mbali mbali na pengine tarehe zao za kuzaliwa na za kuondoka ulimwenguni.

Shekhe ameanza kitabu chake, kama ilivyo kawaida yake kwa dua za ushairi. Hii ni fani nyengine ya shekhe. Yeye ni mshairi mkubwa si kwa lugha ya Kiswahili pekee bali hata kwa lugha ya Kiarabu.

Katika utangulizi wake yeye mwenyewe, kwa kifupi amewataja wale Makhalifa watano na muda wao wa kutawala. Yaani Seyyidna Abubakar, Seyyidna Umar, Seyyidna Uthman, Seyyidna Ali na Seyyidna Hassan.

Maana ya jina lake, ni mzuri wa kila kitu, alipewa jina hilo na Mtume mwenyewe ingawa wazee wake walimwita Harb (vita). Lakini siku zote Mtume alikuwa akipendekeza kwamba mtoto apawe jina zuri.

Jina hilo la Hussein, alikuwa hajawahi kuitwa mtu mwengine kabla ya yeye na baada ya kuzaa alipewa lakab ya Abu Abdalla.

Alizaliwa katika Mwezi wa Shaaban katika mwaka wa nne Mtume kuhamia Madina. Aliadhiniwa, akafunguliwa koo na pia akafanyiwa akia ni mwenyewe Mtume na alinyonyeshwa na Bibi Ummul Fadhl.

Seyyidna Hussein alisoma Quran kwa baba yake kisha akamaliza kwa bwana Abdurahmanis Sulamy. Msomo huu ulipokewa kwa Bw. Hafsi Bin Suleiman na yeye alipokea kwa Bw. Asim Najud na yeye alipokea kwa Bw. Abdurahmanis Sulamy na yeye alipokea kwa Seyyidna Ali, na yeye alipokea kwa Mtume Muhammad (S.A.W.).

Seyyidna Hussein alikuwa na wake wane. Watoto wake waliojulikana ni saba, watano wa kiume na wawili wa kike. Alipofariki alikuwa na umri wa miaka 57 na kauli yenye nguvu yasema kwamba katili aliyemkata kichwa anaitwa Shimr bin Dhiljawshan.

Kitabu hiki cha Tareikh ya Seyyidna Hussein kimetoka karibu na Muharram, wakati ambapo ndugu zetu wa Kiithnashary huomboleza mauaji ya Karbala.

Lakini hichi ni kitabu cha kila Islamu kwani ndani yake kimekusanya mambo mengi ya tarehe ingawa ni kitabu cha kurasa 46 pekee.

Bei ya kitabu hichi ni shillingi nane, na kwa muda huu nadhani kimeshasambaa Mombasa nzima katika maduka yote ya vitabu.

Kwa hivyo iwapo wakaa mbali na Mombasa fanya kila bidii ukiagizie. Lau utakifungua kitabu hichi na hapo hapo uletewe kikombe cha chai, basi chai hiyo itapolea. Maana mujarab wa kusoma mstari wa kwanza, katu hukiweki chini mpaka umekimaliza.

Ni kweli haya mambo na wenyewe si makeke na mayowe. Naam nazi kushindana na mawe zimekwisha umriwe.

WAZIRI MDOGO wa Biashara ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tawi la Kanu Mombasa na Mbunge wa Mombasa ya Kati, Bw. Shariff Nassir akihutubia Nairobi katika chakula cha mchana kilicho andalia na Wizara yake kwa heshima ya Ujumbe wa Biashara kutoka Pakistan. PICHA: KENYA NEWS AGENCY

SAUTI ZA WASOMAJI

COASTWEEK Sanduku La Posta 87270 Mombasa KENYA

WASIOJIWEZA SASA WAKUSANYWE

RAIS WETU mpendwa Bwana Daniel Arap Moi anastahiki pongezi za wananchi wote kwa kufanya utaratibu na kwa busara sana akaweza kuandaa harambee ya kuchangia ndugu zetu wasiojiweza wa nchi hii ambapo jumla ya shillingi millioni ishirini zilikusanywa hapo tarehe nne Oktoba mwaka huu.

Makampuni na watu mbali mbali wakiwa wafanyi biashara, matajiri, mashirika ya umma, idara na wizara za serikali, hakuna sehemu iliyobaki ambayo haikupeleka mchango wake kwa ukarimu. Huu ni moyo wa upendo kwa wale ambao Mungu hakuwatimizia baadhi ya viungo katika miili yao, na kwa hivyo wanashindwa kujitafutia riziki pamoja na jamii zao.

Kila aliyetoa mchango, alikuwa na shebaha ya kusaidia hawa wasiojiweza ili na wao waishi kama watu wengine. Na hivyo Rais aliitisha mwito kwa madisii ili wakusanye orodha za wasiojiweza kutoka wilaya zao ili ijuilikane hesabu kamili ya fedha ambazo kila mwezi zitahitajika kwa kuwaangalia watu hawa wasiojiweza. Rais pia alipendekeza kwamba siku za mbele wasiojiweza wajengewe jengo la kuwaendeshea maisha, ili mateso yao ya kukaa mabarazani na kuomba sadaka yamalizike mara moja.

Sasa ndugu zetu wasiojiweza iwapo wataendelea na kupita pita na kuomba sadaka kama linavyofanya kabila fulani hapa mjini Mombasa, hawatafanya jambo la maana. Maana iwapo kuchwa nzima amepata shillingi tano, pesa hizo hazimpeleki popote. Vile vile ndugu hawa ni budi wawe waaminifu wakati wanapojiandikisha kama wasiojiweza kwa tamaa tu ya kwenda kupawa vya bure. Maana humu mijini tushakumbana na wasiojiweza ambao huko makwao wana mashamba. Wengine huomba mchana usiku wakenda wakalewa.

Vilema hawa, viwete hawa, viziwi hawa, mabubu hawa, vipofu hawa siwo wananchi waliowafanyia hiyo Harambee ya Mwaka. Maana hiyo ni Harambee ya kusaidia wasiojiweza na wala si ya kuwatajirisha wale wanaojifanya wasiojiweza.

Serikali yetu yataka iwamwilike sana watu hawa maana wengine ni wadanganyifu. Hawapendi kumwaga jasho lao. Ukupigao ndio ukufunzao.

TWAMLILIA ALI GUNDA

TUMESIKITIKA upeo kwakufiliwa na mwana chuoni wa kuchagua Sheikh Ali Bin Seneda (Gunda).

Ni jambo muhimu sana kujua malezi na masomo ya chuo cha Quran ambacho marehemu alisoma, lakini kwa wakati nilionao sitobahatika kueleza hayo yote.

Pamoja na hivo hilo halitoniwasa nimi kusema machache kuhusu marehemu. Marehemu zamani tunapotaka kumjua Sheikh wake halisi tutasema ni Sheikh wetu mtukufu Sheikh Muhammad Bin Ahmad Bin Ali Al-Lamy (Sheikh Bereki).

Kwa mwana chuoni huyu marehemu alisoma na akakomaa katika elimu za sheria ya Uislamu kadhalika elimu za adabu ya kiarabu. Alikwa mtiifu kwa Sheikh na kwa sababu hiyo Sheikh wake alimpenda upeo na marehemu alikua ni mwanafunzi wa kwanza alopata ruhusa kusomesha, kuhutubia na kuswalisha kuteka kwa Sheikh wake.

Vitu muhimu vakujivunia na marehemu nikwamba ni mtu wa kwanza katika ukanda wa pwani wa Kenya aliojitokeza si, kusoma na kusema tuu kwa lugha ya Kiarabu lakini ni mtu wa kwanza aloweza kuzitetemesha membari za misikiti na majukwaa ya kidini kwa hutuba zilokua zikisin'nyangwa kwa uhodari wake na munasaba wa kikao, kwakiwango cha juu sana cha lugha yakiarabu.

Marehemu amewahi kupeleka vijana wengi nchi mbali mbali kwa masomo ya juu.

Musa aliweza kufanya mengi kwa kumpata Harun na marehemu kama alipata wasaidizi wenye ujuzi wa kutosha na hima zenye ikhlas angalipata kubahatika zaidi.

Katika wanafunzi mashuhuri wamarehemu ni Ndugu yetu mpendwa, Ustadh Alwy Kassim Alalawy.

Diwani Maalum Harith Swaleh, LAMU.

HEKO MADIWANI

NIKIWA kama mzazi, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Chama cha Wazazi cha Skuli ya Serani, natoa pongezi kwa mwenyekiti wa chama hicho na pia Mjumbe wa Mombasa Kaskazini Mhe. Said Hemed kwa kupitishwa maombi yake katika baraza la Manispaa ya Mombasa la kutaka zile afisi za Afisa wa Elimu wa Manispaa ya Mombasa kugeuzwa madarasa ya nane na ya tisa hapo mbeleni wakishaguria afisi zao mpya.

Shukurani na hongera pia kwa Madiwani wote wakiongozwa na meya wao kwa kuitia manani na kuipitisha kwa sauti moja hatua hii ya maana sana. Kwa hakika hapa tunaweza kusema kwamba madiwani wetu wamecheza kama pele.

Sasa nawarudia wazazi wote wenye watoto katika shule ya Serani, baada ya kusikia tangazo hili wao wamejiandaa namna gani?

Iwapo Manispaa imeshaturudishia jengo letu (maana afisi hizo ni katika majengo ya shule ya Serani asiyeyajua haya naasome historia ya Mombasa au nawaulize ambao yeye mwenyewe akiri kuwa wamzidi kwa elimu ya mji huu) lakini haijatupa vifaa vinavyofaa kwa elimu ya upili (sekondari). Na pia wazazi wafahamu kwamba majengo hayo kabla ya kuanza kusomewa ni lazima yarakibishwe ili yawe na sura ya madarasa.

Nataka wazazi wa Serani wafahamu kwamba kupata majengo hayo, ni sawa na kupata maana kutoka mbinguni kwa sababu hivi tunavyozungumza hakuna hata skuli moja ya Manispaa ambayo iko na majengo ya tayari ya kufanya kidato cha kwanza na cha pili.

Kwa hivyo nawataka wazazi wote wakati utakapofika wa kuyarakibisha majengo hayo waoneshe ya ghera kuliko ile ghera wanayoonyesha katika kupamba veli na kuandaa karamu kubwa kubwa ili tuweze kutayarisha majengo ambayo kweli yanaweza kutoa elimu ya kujitegemea kwa vijana wetu siku za baadaye.

Na pia nachukua fursa hii kuwaalika wazazi wote kwenye ile shughuli yetu ya kila mwaka yaa ni "Siku ya Wazazi na pia Kutoa Zawadi" ambayo itafanywa hapo hapo Skuli ya Serani tarehe December 2 mwaka huu. Njoni kwa wingi musikie maoni yetu kwa maendeleo ya siku za mbele ya watoto wetu.

Sheikh Ali M. Yumen, MOMBASA.

Coastweek ★★ SWAHILI CROSSWORD NO. 103

JEMBE

UNGA SAFI NO. 1



KWENDA KULIA:

1. Ufundi, maringo
5. Moja, kwanza
7. Malizikia
8. Osha, safisha
10. Rangi kama pambo
13. Linda shamba
14. Wewe
16. Ndani kwa Kimombo
17. Mamlaka, utukufu
18. Afunga ndoa
20. Mwanamke aliyeolewa
21. Neno la kukanusha
23. Mchezo haramu

KWENDA CHINI:

1. Mwenye nguvu
2. Chukua kitu kwa mtu kisha kukirudia
3. Si pm
4. Paa dogo
6. Lalia mayai
8. Kiungo cha maneno
9. Kifaa cha maandishi
11. Ibwage juu ya meza
12. Kinyume cha nyembamba
15. Ukoo, jadi
19. Ghera, juhudi
22. Kama No. 3 kwenda chini

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 101

[1] Hassan Jumaan Awadh, Sanduku la Posta 81854, Mombasa,

[2] May Sezuah, Sanduku la Posta 85816, Mombasa,

[3] Mr M. K. Kumenzwa, Sanduku la Posta 80353, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 101 —

KWENDA KULIA:

1. DUKUDUKU, 5. LA, 6. RADI, 7. RADHI, 8. KOBA, 9. RWANDA, 12. AA, 14. DUMA, 15. IBURA.

KWENDA CHINI:

1. DHARURA, 2. KONDOA, 3. DARI, 4. ULIMBO, 8. KANDA, 10. WAHI, 11. NYAU 13. WAA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270 Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 20.11.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.